Ilani: Mawasiliano ya haki ya kijamii nyakati za kidijitali

Ilani hii yenyi kukubaliwa na washirika wote ni matokeao ya mkutano uitwao « Mawasiliano kwa ajili ya haki ya kijamii kwa wakati wa kidijitali » iliyoendeshwa tarehe 13 hadi 15 septemba 2021

Harakati ya kiekumene

Tarehe 16, mwezi wa 9 wa mwaka 2021

Kongamano kuhusu kijiditali

Tafazali ugawanye maandiko hii kwa wengine

Ilani hii ni matokeao ya kongamano iitwayo « mawasiliano kwa ajili ya haki ya kijamii kwa wakati wa kidijitali » iliyoendeshwa tarehe 13 hadi 15 septemba 2021. Kongamano ile ili kuwa ikilenga kuchunguza changamoto za mawasiliano za kigijitali yenyi kuhusu haki ya kijamii na kutambua fursa za kuchukua hatua za pamoja kati ya mashirika za kidini, shirika la kiraia, wasomi, vyombo vya habari na makampuni za kiteknolojia.

Kongamano iliandaliwa na Baraza la Makanisa za Ulimwengu (Conseil œcuménique des Eglises) na Chama ulimwenguni cha mawasiliano ya kikristo (l'Association Mondiale pour la Communication Chrétienne)na kwa msaada wa Pain pour le monde (Brot für die Welt), wa Kanisa la Kiinjili la Ujeremani (EKD), wa Chama cha Makanisa na Misioni za Kiprotestanti wa Ujeremani (Evangelicshe Mission Weltweit, EMW) na wa Shirikisho la kimataifa la vyama vya wanafunzi wa kikiristo (Fédération universelle des associations chrétiennes d'étudiants).

Tukio hilo lilikutanisha watafiti, ujuzi kutoka mikoa mbalimbali na kutoka jamii zisizojiweza kijamii na kimali na ambazo zilitengwa, maonyesho ya wataalamu kuhusu mwenendo wa kiuchumi na kisiasa na pia tafakari za kanuni za maisha na kitheolojia kwa ajili ya kuleta mchango wao kwenyi mkutano wa COE ambao utafanyika mwezi wa septemba 2022.

Muktadha ulimwenguni

Teknolojia za kidijitali zinabadilisha ulimwengu pamoja na mahali mingi ambamo tunaishi na kukomaa.

Teknolojia hizo zatusaidia kupata namna ya kuhojiana, na kutupasha habari nyipya, kubadilka duniani, kukinga ustahili na haki za binadamu na pia kusikilisha kwa wenggine maoni yetu.

Hizo teknolojia zinaunda njia nyipya za kukutanana kati ya watu zikifuta mipaka iliyokuwepo ya muda na nafasi.

Zinaweza kuwa vyombo shujaa vya kukutanisha wengine, vya ushirikiano, vya mafunzo, vya kuhojiana, vya kutafakari, vya kuumba mawazo mapya na pia vya maelewano.

Ila, hata kama teknolojia za kidijitali zinakuwa ni nzuri, zinakabiliwa pia na changamoto.

Majukwaa ya kidijitali hutumiwa pia kwa kutawanya kwa hiari habari zisizo za kweli na za chuki, na pia habari zenyi kuzorotesha ustahili na haki za binadamu

Kampeni za kidijitali za habari zisizokuwa za kweli ao *fake news*, zenyi kutegemea siasa hukiuka mwenendo bora wa demokrasia na upashaji habari yenyi kuheshia jukumu.

Hata kama mitandao za kidijitali zinapana uwezo usio na mipaka wa uhuru wa kujitetea, uwingi wa mashirika zenyi kuongoza kwa hiari yazo teknolojia za kidijitali huharibu zaidi uwezo wa kutawanya fikra zenyi kuwa umbalimbali na pia maoni.

Mawasiliano inaendelea zaidi kupitia kwenyi njia za kibinasfi ambazo huuzishai watu ndoto za kuwapa ushujaa na uwezo wa kidemekrasia. Ila kwa kweli njia hizo za mawasiliano zinahatarisha uwepo wa data na kupitisha bure wakati, hali ambazo wataalamu huita ''akiba ya uelekevu''.

Data toka mashirika za kibinafsi zinaombwa sana, zinakusanyishwa na pia zina shikiliwa na vikundi fulani kwa ajili ya kunyanyasa watu kiuchumi na kisiasa.

Ufuatiliaji, utengaji na uwekaji na kutumiwa kwa njia za kiaskari ni vitisho vikubwa kwa nafasi za kidijitali.

Zikimaanisha dalili zinazoendelea za kumbukumbu ya nyakati za ukoloni, ubaguzi wa rangi na usawa wa nguvu za kimfumo, kanuni zingine zilizoundwa bila kuonyesha ukweli wa mabo huzidisha ukosefu wa usawa usawa na ubaguzi uliopo.

Janga la COVID-19 pia linakomalisha ukosefu wa usawa kati ya watu. Watu ambao hawajajumuishwa katika nyanja ya dijitali wanaona kutengwa kwao kunaongezeka pamoja na kuhamishwa kwa mafunzo mtandaoni na uchumi. Masuala ya usalama wa mtandao yanaongezeka, hasa zaidi katika sekta ya afya.

Mitazamo ya kitheolojia

Mabadiliko haya ya jamii yanakomalisha shida zachinini chini ambazo ambazo jumuiya ya kiekumene imekuwa ikiyafanyia kazi miaka mingi iliyopita : Tukitaja mamlaka, haki, usawa, ushirikishwaji, ukomalishaji wa shirika za binadamu zenyi kudumu, njia za kusikika sauti za pembeni na pia utu wa binadamu.

Wakati tulikuwa tukitafuta kujibu maswali yaliyotokana na mabadiliko ya kidijitali, mila nyingi za kidini hutoa mafundisho ya kinaganaga kuhusu maana ya uwepo wa binadamu na kuishi maisha ya haki ambayo ni sehemu ya uumbaji.

Kuna vipengele viwili visivyoweza kutenganishwa na ni ya lazima vichukue jukumu kuu katika mawazo ya kitheolojia juu ya haki ya kidijitali: uhusiano na kuathirika (ao kuishi katika mazingira ya magumu).

Katika imani ya Kikristo, uumbaji kwa mfano wa Mungu hutoa heshima ya asili kwa kila mwanaume, mwanamke au mtoto (Mwanzo 1:27). Binadamu ameumbwa ili aendeshe mahusiano na aweze kushirikiana na kuwasiliana. Tumeitwa kuwajibika na kutunza uumbaji wa Mwenyezi Mungu

Katika Yesu Kristo, Mungu aliweza kujiajibisha na kushiriki maisha yetu ya kibinadamu. Kwa hiyo, uumbaji na mwanadamu lazima wabaki katika moyo wa mawazo na mahangaiko yetu. Kuajibika hii ya pamoja hutusukuma kulinda haki za mtu binafsi na za pamoja na kutumia teknolojia za kidijitali kwa ajili ya ustawi wa binadamu. Kuchagua kuwapenda wa maskini na walio katika hali ya magumu ginsi inaloonyeshwa wazi katika Biblia (Mt 5) linaelekeza mawazo yetu tukiona kama tumenyimwa kuwasili habari na mgawanyiko wa kidijitali ulimwenguni.

Tumealikwa kujitoa katika njia ya haki, amani na ulinzi wa viumbe vyote.

Tumeitwa kushiriki katika utume wa Mungu kusudi kila mtu apate uzima na akuwe nao kwa uwingi, hata katika nyanja ya kidijitali (Yn 10,10).

Munamo mwaka wa 2022 Jumuiya ya Kiekumene itakusanyika huko Karlsruhe (Ujerumani) kwa ajili ya Mkutano wa 11 wa Baraza la Makanisa Ulimwenguni, litakalofanyika katika ulimwengu unaogubikwa na aina nyingi za dhuluma na mateso ya sehemu kubwa ya watu wake, ya viumbe vyake na hata ya udongo yenyewe.

Lakini pia ni ulimwengu ambao tunashuhudia harakati za mabadiliko, za haki na pia za matumaini.

Masuala na changamoto

Uwekaji kidijiti katika aina zake nyingi husisimua maswali mapya kuhusu utambulisho na uhuru wa binadamu. Kinachohusika sio tu mshikamano wa kijamii, bali pia utu wa mwanadamu.

Uwepo wa kidijiti husisimua pia maswali ya haki ya mazingira, hasa kuhusu unyonyaji wa rasilimali na mchoko uliopangwa wa teknolojia za kidijitali.

Wahusikao katika siasa, utamaduni na mashirika za kiraia, wasomi na jumuiya za imani wote wanajitahidi kufanya vizuri iwezekanavyo.

Kwa ajili yakukabiliana na changamoto na kutumia fursa zinazojitokeza katika enzi ya kidijitali, ni lazima tuchukue mbinu za ushirikisho , za kujumuisha na ya kiujumla ambayo sio tu ya kimataifa na baina ya vizazi, bali pia mbinu zenyi kuzingatia samani takatifu ya haki ya kijamii.

Hii inatufanya tujiulize swali lifuatalo: tutafnaya je kwa ajili ya kuleta ikolojia wa mawasiliano na habari unaozingatia kanuni za haki ya kijamii kama vile ushirikishwaji shirikishi, uhuru, usawa, uendelevu wa maisha na mshikamano? Baadaye, mfumo huu wa ikolojia utakuwa:

• Kuwezesha kila binadamu kutekeleza kikamilifu haki za binadamu, haki za kiraia na wajibu wake;

• Kuimarisha hali ya uwepo na ushiriki wa pamoja;

• Kuhimiza mashirika na miungano inayojenga uaminifu, uwajibikaji na kuaminiana;

• Kufanya kazi za kujumuisha na kusherehekea sauti zisizokuwepo, zenyi kupuuzwa, zenyi kunyamazishwa na zile zenyi kutengwa katika ulimwengu wa kidijitali,

• Kupiganisha ubaguzi wa wazi na wenyi kufichwa, ubaguzi wa rangi, ubaguzi wa kijinsia na itikadi kali katika teknolojia ya kidijitali,

• Kuonyesha mshikamano na idadi ya watu wanaohudumiwa bila kutotafuta faida wala mamlaka;

• Kuhimiza majukwaa yenyi kufundisha watu kuishi pamoja, mshikamano, ushirikiano na kuungana kwa ajili ya ustawi wa watu na dunia waishimo;

• Kuhimiza majukwaa ya uwazi ambayo yanayozungumza kwa uwazi kuhusu samani yanayowasukuma kukutanana,

• Kufaidika na teknolojia kamilifu katika uchumi wa kidijitali na kushiriki maarifa na data kwa uhuru.

Tumeainisha changamoto za muhimu zifuatazo:

Mgawanyiko wa dijiti. Tunakabiliwa na migawanyiko ya kidijitali ya kila aina: kiuchumi, kijiografia, rangi, elimu, kijamii, ngono (jinsia), kizazi, kitamaduni, kiteknolojia na kimataifa. Pia kuna mgawanyiko wa asili ya kidigitali.

Mgawanyiko huu wa kidijitali unaonyesha utata wa haki ya kijamii katika enzi ya kidijitali na hitaji la kufikiri kati ya makutano yanyi kukusanya watu toka mazingira mbalimbali. Haki ya kidijitali inahitaji haki ya kijinsia, haki ya hali ya hewa, haki ya kiuchumi, haki ya rangi na mengine mengi.

Ukaribiaji. Tatizo kuu yenyi mara nyingi huwa ni uhaba wa nafasi ya digital yenyewe. Jambo hili linaficha kuonyesha kwa uwazi tofauti iliyoko kati ya uchumi wa chini, wa kati na uchumi wa hali ya juu ndani ya nchi moja. Hakuwezi kuwa na ukaribiaji wa kweli bila ufikiaji wa vyombo ya mawasiliano (uwepo wa umeme na Mtandao, vifaa vya kiteknolojia) na vyombo, data, mipangilio maalum na yaliyomo ya dijiti kutoka kwa muktadha wa kitamaduni wa ndani, ambayo huongeza mifumo ya kisheria na kiuchumi. rasilimali zinazoruhusu ufikiaji na uundaji wa makazi katika eneo hili.

Mashurti za ukaribiaji zinakuwaka na matokeo dhidi uhusiano wa nguvu na usambazaji wa rasilimali. Kwa hivyo, ufikiaji wa teknolojia ni sababu na matokeo ya magawanyiko wa dijiti.

Uwezo wa kumiliki ni jambo la muhimu kwa watu wenye ulemavu. Lakini ushirika wao kwenye shughuli za uchumi uliboreshwa kupitia vyombo vya kidijitali. Na kushiriki kwao katika shughuli za kiuchumi umeboreshwa, pia wanaburudika na wanakutatana kijamii na watu walio wengi. Hata hivyo, kufikilia uboreshaji kamili ya uwezo wa watu walemavu kumilki ingali inakumbwa na vitisho vya utajiri wa mataifa.

Nafasi ya uma : Ni mahali ambako Mataifa na kundi la watu hukutanana kwa ajili ya kuhojiana, na pia ambako raia (ikiwemo pia vyombo vya upashaji habari) wanaweza kuchangia mawazo, nia zake, na kushiriki kupitia njia za kidemokrasia. Kuingia katika kidijitali hupana uwezo wa kuongeza eneo la mahali pale, ila vizuizo fulani vya kijiditi vyaweza pia kupunguza unene wa mahali pale pa mahojaino kati ya watu na mataifa.

Uhaba wa usawa kati ya watu : Uwezo wa kumiliki, wa kutumia na wa kutafakari kuhusu data za kijiditali huzingatiwa na mashisrika fulani na pia sehemu fulani za dunia. Viongozi wa inchi wanaweza pia kujihusisha sana katika umiliki na utumiaji wa data hizo.

Elimu : Mafunzo ya kijiditali yenye kuelekea kujiswali na kutafakari kuhusu habari na wapi zilitoka ni jambo la muhimu kwa kila binadamu. Mara mingi kifikilia ujuzi huo hulingana na umri, elimu, lugha, jinsia, mahali mtu anapoishi na mipangilio ya makazi kati ya wanawake na wanaume katika shirika lao.

Sheria ya kijinsia : Wanawake kufaidika na kidijiti kwa njia binasfi, kwenyi elimu na pia kwenyi uchumi. Ushirikisho kamili wa kidijiti inaweza kusaidia kushiriki kwao kinaganaga katika hali zote za maisha. Ila vizuizo vya kijinsia vilivyopo kati ya wanaume na wanawake huzuia pia ushirikiano huo.

Kulingana na utawanyashaji wa kidijitali, wanawake na pia mabinti hujikuta wanakabiliwa na hali ya unyanyasi wa ngono, wanachunguliwa zaidi, na pia wanatukaniwa na kuchukiwa mtandaoni. Hali hii yaweza kugeuka kuwa ujeuri. Matokeao ya ujeuri mtandaoni ni kwamba ina sukuma wanamke kuwa kimya na kuwashurtisha kujiondoa katika mawasiliano ya kijiditali.

Heshima ya maisha ya mtu binafsi na usalama : Matatizo kuhusu utumiaji wa data na kujiingiza katika maisha ya mtu binafsi hujitokeza wakati serikali iazibiti dijitali kiolela, wakati sheria na

kanuni za inchi kuhusu dijitali hazikamilke, wakati intaneti inaktwa kwa ajii ya kuzuia raia wasipinge mipango ya kiserikali kupitia mtandao, ao wakati serikali inashurtisha kanuni za kuchungua yote yapitayo na yasemwayo matandaoni bila sababu.

Jeshi: Teknologia za kijiditali ni uwezekaji wa kijeshi, na kiisha zinatumiwa sana kiaskari, jam,bo ambalo linaweza kuongeza hatari mengi wakati wa mizozo.

Shurti za kutimiza kwa ajili ya kufilikilia mahojiano ambayo inasaidia kutimiza sheria ya kijamii wakati wa kidijitali

Ni vigumu sana kufanya lolote bila mawasiliano yenyi kukamilika, haizuru iwe njia gani ya utumiaji wake (ujeuri dhidi ya wanawake na watoto, umaskini, utatuaji wa mizozo, kujitemegemea binafsi, ubaguzi wa kabila, uhamisho, haki ya kumiliki kazi, kahi za watu wa kiasili, afya, udongo, hali ya hewa).

Kulingana na ile, tunapashwa kushirikisha kikamilifu watu wote kwa ajili ya kuunda teknolojia za kijiditali zenyi kurahisisha maisha, heshima za utu na sheria pahali ya kuvizuia.

Tunahitaji kanuni zenyi kuruhusu kila mtu kushiriki katika mjadala ya wazi wazi, yenye kutoa mwangaza na ya kidemokrasia, na pia kumiliki bila kukaziwa habari na ujuzi zenyi kufikisha watu kwa maisha ya pamoja katika amani, kujitoshelea binafsi, upendo wa inchi na kujiaminia binafsi na pia kuaminia wengine.

Chanzo cha kanuni zile hupatikana katika historia ya haki za mawasiliano na ambazo zinatarajia ulimwengu ambamo :

- Kila mtu ana haki ya kuhojiana, kutangaza habari na kuchangia ujuzi. Hii inapitia katika ufikiliaji wa watu wote bila tofauti kwenye vyombo vya mahojiano na uhuru wa kuzungumza.
- Kila mtu ana haki kushiriki kwenye shirika la upashaji habari na mawasiliano, mingi zaidi kati ya vikundi vilivyo na watu wachache ao zenyi hazijiwezi. Hii inapitia katika uongozi bora kwa faida ya watu wote na ambamo kila mtu anashirikishwa kwa vyombo vya utawanyaji wa habari na vikundi vya kidigitali.
- Kila mtu ana haki ya mahojiano yenyi kuhusu watu wote bila tofauti na yenyi haifaidishe kipekee ao kuzuru mtu fulani. Hii inapitia kwenyi njia za heshima kwa kanuni za upashaji habari, shurti za kueleza kile mtu alichoona na uwezo wa kuomba kisahihishwe wakati ambayo maneno iliyopitikana iligeuzwa wakati wa kuieleza.
- Kila mtu ana haki ya utu na heshima. Ile hupitia katika ukweli kutumika vizuri kwa vyombo vya habari na vikundi vya dijiti.
- Kila mtu ana haki ya kuheshimu maisha yake binafsi na maarifa ya kufikia habari zenyi kumuhusu, ingawa hakutajwa katika ukeukaji wa haki za binadamu ao katika mambo ya uhalifu. Haki zile zenye kuangalia kibali cha kidigitali cha kila mtu hupitia kwenye ngazi za kisheria na amabazo zinachunga haki ya heshima kwa mtu binasfi na ukingo wa haki za binadamu zibakie imara.

- Kila mtu ana haki ya kuishi utamaduni wake na lugha yake. Hii inapitia katika utengenezaji wa nafasi ya uonyeshaji ya utamaduni na lugha kwa ajili ya wote na pia uwezo wa kufikilia na kumiliki vyombo vya habari.
- Kila mtu ana haki ya kupewa ujuzi kuhusu mahojiano na kujifundisha utumiaji wa vyombo vya habari. Hii kupitia katika vipindi vya mafunzo yenyi kuambatana na utamaduni na pia kuongeza ujuzi ya lazima (mazungumzo, mahojiano, kusikiliza, kufungua moyo na kutafakari).
- Kila mtu anafikilia vyombo vya kutoa moto vyenyi kudumu kwa ajili ya kutumikisha vyombo vyake vya kijiditali. Hii hupitia katika ufikiliaji kwa wote ku teknolojia kama vile ya moto inayotolewa na jua ao na mpepeo.
- Kila mtu ana haki ya vyombo vyenyi kulingana na hali yake ya kiuchumi ao umiliki wa vyombo vya uma vyenyi kushimikwa mahali penyi kulindwa. Hiyo inapitia katika rasilimali ya kiuchumi na pia kwenye « haki ya utengenezaji ».

Chama chenyi kuleta mabadiliko

Kwa ajili ya kufanya sheria ya kijamii kuwa kamilifu, ni sherti kuwe chama cha kubadilisha watu, mashirika za watu, masomo, vyumba vya habari na shirika la raia- vikiwemo mashirika za kiimani. Yafaa pia siasa na mipango ya kiserekali yenyi kuwa wazi na yenyi kukubaliwa na shirika la raia, lakini pia ikuwe yenyi kutetea utu wa watu, haki za binadamu na kanuni za kidemokrasia.

Haki za msingi haziwezi kujitimiza pekee yake ao kulingana na kupitia mapenzi mema ya mashirika za kidijitali. Ni vizuri pia kutafuta msaada na agano toka shirika la raia – wakiwemo pia makanisa na mashirika za kiimani na za kisiasa, wana sayansi na uchumi- kwa ajili ya kuhakikisha na kukinga haki za watu wakati huu wa miaka ya kidijitali na kufanya iwezekanavyo ili nafasi ya kidijitali itumiwe na kufaidia watu wote.

Ni kwa ajili ya kupekua maswali haya yote ndiyo maana kongamano iitwayo « mawasiliano kwa ajili ya haki ya kijamii kwa wakati wa kidijitali » iliweza kuandaliwa : Kujifunza na kuchangia mawazo kuhusu namna teknolojia zitaweza saidia binadamu mnamo siku zitakazo kuja. Kongamano haikushurulikia tu serikali na mashirika makubwa.

- Tulisisitiza juu la lazima ya uwepo wa kanuni za kushirikisha watu wote, za heshima na za usawa
- Tulisisitiza umuhimu wa haki ya kuwasiliana kwa watu na jamii zisizojiweza ulimwenguni.
- Tulihakikisha ya kwamba haki za binadamu katika eneo la kidijitali zapashwa kupatikana pia katika eneo za uma.
- Tulikataa mafasirio yoyote kuhusu ujeuri unaotendeka kupitia mtandao na yenyi kwenda kinyume na Injili
- Tulikubaliana wote juu ya umuhimu wa haki za mtoto na juu ya kuwapa vijana wakati wa kutimiza jukumu zao za kushiriki katika madadiliko ya kidijitali yetu.
- Tulisisitiza ya kwamba data zote ziwekwe tayari kwa vitumiwa kwa mafaa ya watu wote (wakati hazihusu maisha ya mtu binafsi)

- Tulisistiza umuhimu wa kuongeza jukumu na uwazi wa mashirika makubwa zinazo uwezo wa kushawishi na kuongoza hotuba za kisisisa.
- Tulitia mkazo kwenyi hatari ya *darknet* inayohusu kazi zisizokuwa halali na zenyi kuwa na uharibifu kama vile kuuzisha viungo vya mwili ya mtu, kuwatesa watu, unyanyasi kupitia katika njia za ngono, uchuruzi wa mabunduki na pombe makali za kulevya na hata kuandikisha watu kwenyi mashirika za jidihada kali.
- Tulikubali uwezo wa nafasi za kidijitali kama ni vyombo vyenyi kuruhusu jamii za watu wenyi kunyanyaswa ili wateteye utu wao na kuzungumuza.
- Tulishawishi na kusukuma jamii ya kiimani ifanye yote iwezekanayo kusudi watu wasiojiweza wafaidike na kupata kidijitali iliyo ya haki.

Kwa ajili ya kukabiliana na changamoto na kufaidishwa na uwezo wa teknolojia za kidijitali, tunapashwa kuwa na eneo la kidijitali lenyi kubaki daima na lenyi kutumiwa na wote. Kwa hiyo, mstari wa mbele utashikwa na haki za msingi, kila mtu akubali jukumu lake na pia umoja.

Tutashirikisha wana siasa, mashirika za shirika la raia na vikundi vya kidini kwa ajili tupate mahali na vyombo vya habari vyenyi kuhusisha na kushirisha watu wote na ambazo zinategemea sheria ya kidijitali, zenyi kunenepesha ao kupanua nafasi ya kukutanana kwa watu walio wengi na kutafakari kuhusu maisha ya siku zijazo.

Tutahimiza ukosoaji wa kitheolojia na wa kimaadili dhidi ya nguvu zenyi kutumia nafasi ya kidijitali ambayo hairuhusiwe na ya kibiashara.

Tunapinga upinzani wowote yenyi kuchochewa na dini dhidi ya nguvu zenyi kuzoofisha ustahili na utilifu wa binadamu katika nafasi ya kidijitali.

Kusudi ya kuendelea na mipango ile, tunajitolea kutayarisha agenda ya hatua ambayo italeta ukweli huu uliovumbuliwa upya kuwa hai katika vipindi mbalimbali.

Tutaendelea kuenda pamoja ili sheria itiririke kama maji na ukweli uwe kama kama kisima ambacho hakiwezi kamwe kukauka.

(Amosi 5 :24)

Tarehe 21 septemba 2021

Utangazaji wa ilani inaruhusiwa na Creative Commons CC BY-NC-SA 4.0 (Kupewa – Siyo kwa utumizi wa kibiashara – Ya kugawanya kulingana na shurti Ulimwenguni 4.0). Munaweza kuchapisha upya, kugawanya upya na kulinganisha maandiko haya kwa maffa isiyo ya biashara, ila yafaa kujisha chanzo chake. Kama unarudilia, unageuza ao unaongeza yaliyomo ya maandiko haya, msaada wako wapashwa kugabuliwa kulingana na ruhusa ya utangazaji tuliotaja hapo mbele. Mafasirion mengi kuhusu ruhusa ya kutangaza inapatikana hapa : https://creativecommons.orglicences/by-nc-sa/4.0/deed.fr

About the language:

Swahili is one of the four languages of the Democratic Republic of the Congo, along with Kikongo (Kituba), Lingala, and Tshiluba. French is the official language and is widely used in administration and education. Swahili is widely spoke in the eastern part of the country, according to Translators Without Borders.

About the translator:

SAMWAKI is a rural women's organisation based in South Kivu, the Democratic Republic of the Congo, which seeks to end gender-based discrimination and promote rural development. Samwaki, according to its website, "works with 250 grassroots women's organisations to increase women's capacity to participate in local socio-economic development. SAMWAKI created rural community radio programs and all-women listeners' clubs to give women both a forum to share their experiences, and access to information. SAMWAKI also uses their platform to provide training and seminars to community leaders and journalists."